# PENPLUS SCHOOL BASED EVALUATION TEST
# DARASA LA SABA MUHULA WA TATU -

PENPLUS MK-3

# KISWAHILI

*Muda: Saa 1 Dakika 40*

***Jaza nafasi 1-15 kwa kuchagua jibu sahihi.***

Hapo zamani za zama __1__ kijiji cha Pendaraha __2__ mtu __3__ na __4__ yake. Mtu __5__ alikuwa __6__ sana kwa staha aliyokuwa __7__. Aliwaheshimu watu wote, wakubwa kwa wadogo. wake __8__. Siku moja alifanya __9__ ambalo liliwakera wanakijiji __10__. Kioja __11__ kilihusu __12__ __13__ kijana wa kiume aliyewaachilia ng'ombe kuharibu mimea yake. Sifa yake ilichafuliwa zaidi __14__ kifungo cha maisha __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kwenye | B. kati ya | C. katika | D. ndani ya |
| 2. | A. paliishi | B. palikuwa | C. palikua | D. palitukia |
| 3. | A. moja | B. mmoja | C. pamoja | D. mumoja |
| 4. | A. alaa | B. nyumba | C. jamii | D. aila |
| 5. | A. huo | B. huyo | C. huu | D..huyu |
| 6. | A. akiheshimiwa | B. akiheshimu | C. akimheshimu | D. akiwaheshimu |
| 7. | A. naye | B. nao | C. nayo | D. nazo |
| 8. | A. na | B. bali | C. pia | D. kwa |
| 9. | A. jambo | B. chambo | C. njabo | D. mambo |
| 10. | A. yote | B. chote | C. wowote | D. wote |
| 11. | A. wenyewe | B. chenyewe | C. chenye | D. lenyewe |
| 12. | A. maafu | B. maasi | C. mauaji | C. maafa |
| 13. | A. cha | B. ya | C. wa | D. la |
| 14. | A. alipohukumiwa | B. alihukumiwa | C. atakapohukumiwa | D. alipohukumu |
| 15. | A. korokoroni | B. gerezani | C. rumande | D. mahakamani |

***Jibu maswali kulingana na maagizo uliyopewa***

16. Ni nini ukubwa wa:-
**Nyumba yake ni ya fahari.**
A. Jijumba lake ni la fahari
B. Kijumba chake ni cha fahari
C. Jumba lake ni la fahari
D. Jijumba lake ni la fahari

17. Mama alinunua_____ cha majanichai.
A. robota B. kicha
C. kichopa D. kitita

18. Kanusha sentensi ifuatayo.
**Angelima angepata mazao**
A. Asingelima asingepata mazao
B. Asingalilima asingepata mazao
C. Asingelilima asingelipata mazao
D. Angalilima angalipata mazao

19. ***Kamilisha methali ifuatayo***
Ukipewa shubiri usichukue ______
A. yote B. chumvi
C. pima D. upesi

20. Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya -O-rejeshi tamati.
Wanafunzi ambao wana bidii ni bora.
A. Wanafunzi wawao na bidii ni bora
B. Wanafunzi ambao walio na bidii ni bora
C. Wanafunzi walio na bidii ni bora
D. Wanafunzi wenye bidii ni bora

21. "KWA" imetumika kuonyesha:-
**Nimetoka kwa ndugu yangu.**
A. kifaa
B. Umilikaji
C. uhusiano
D. sababu

22. Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendesha.

Micha ata_______ makofi ya kumpongeza mzungumzaji.

A. pigia B. pigiza
C. piga D. pigisha

23. Ni sentensi ipi inayoonyesha **KI** ya namna?

A. Kiatu kile kimeloa maji
B. Akifisha mapema atampata
C. Aliuliwa kinyama
D. Kijiti kile kimevunjika

24. Tambua kivumishi kiashiria katika sentensi hii.

Mwanafunzi huyu mwerevu ameumia vibaya.

A. huyu B. vibaya
C. umia D. mwerevu

25. ***Chagua kiunganishi kifaacho.***

______ ningekuwa na pesa ningenunua gari.

A. Minghairi
B. Kama
C. Lau
D. Ingawa

26. Tumia alama ya uakifishaji ifaayo.

Ukahaba hueneza ukimwi ______ hatuna budi kuupiga vita.

A. . B. , C. ; D. -

27. Mshororo wa mwisho wa shairi unaorudiwarudiwa katika kila ubeti huitwa kibwagizo pia unawezaitwa:-

A. mkarara B. mloto
C. ukwapi D. mizani

28. ______ ni alama ya mkato au tundu inayotobolewa baina ya pua na mdomo wa juu.

A. Ndonya B. Kipuli
C. Kishaufu D. Kidani

29. Kikembe cha sungura ni kitungule. Je kikembe cha mdudu ni ______

A. kitoyo B. kingonyo
C. kidue D. kiwavi

30. Chagua jibu mwafaka kukamilisha sentensi ifuatayo.

Jina ____ la samaki ni nswi.

A. lingine B. jingine
C. ingine D. nyingine

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.***

Katika kitongoji cha ufakara, waliishi wavulana wawili walioitwa adili na Mashaka. Barobaro hao walikuwa marika na pia majirani. Uhusiano huu ulijenga maumala mwema kati yao. Kama jina la kijiji lilivyo wazazi wa wavulana hawa walikuwa wakifanya kazi za kijungujiko mradi mkono upishww kinywani. Hata hivyo, halikuwa jambo rahisi kuzikimu familia zao.

Urafiki wa adili na mashaka haukutetereshwa na umaskini wao licha ya kebehi kutoka kwa wenzao. Wao ulikuwa urafiki wa kufa kuzikana. Walishikilia nidhamu na maadili kikiki. Elimu yao hawakuifanyia mchezo asilani. Walikula kiapo mbele ya wazazi wao kuwa ndio ambao wangekomoa na kukwamua familia zao. Na kwa kuwa safari ndefu huanza kwa hatua, kuwa ungekuwa mwanzo wa kuikomboa jamii nzima. Aidha, waliazimia kuwajengea wazazi wao nyumba za kifahari katika siku za usoni. Hii ilikuwa tunu kwa wazazi wao kwani kote kijijini ufukara hakukuwa na nyumba ya bamba! Wazazi walizugwa.

Kwa kuwa wazazi walifumbwa macho na pambo jipya la maisha hawakuvuta tabasuri kuwa kimumunye huharibikia ukubwani. Maisha ya mashaka yakaingia mashakani. Aliungana na kundi la vijana wasiokuwa na maadili. Akaingia katika uraibu kwanza kama limbukeni na baadaye akawa bingwa. Mihadarati hakuitazama kwa jicho la pili. kadili alivyozidi na ulevi wake ndivyo mkono wake ulivyozidi kurefuka. Akawa hata sindano haioni imekaa pabaya bila yeye kuitwaa. Siku hata siku, mashaka alizidi kupanda ngazi hata akafikia kuwa pwagu.

Adili naye aliendelea kujifunga kibwebwe akiwa na nia ya kufanikiwa maishani. Ni kwa kuwa bidii hulipa, alifaulu kupita mtihani wake hata akapata ufadhili wa kuendelea na masomo. Naye akabarikiwa na Mungu kwa uttifu wake. Akarushwa daraja mbalimbali za fanaka. Akawa mkwasi wa kutajika kote kijijini na nchini. Yeye alielewa kuwa ahadi ni deni na dawa ya deni ni kulipa. Hivyo basi, aliwajengea wazazi wake pandikizi la jumba. Si furaha hizo walizokuwa nazo wazazi.

Siku moja, Adili alikuwa akiendesha gari lake akielekea kijijini, mwendo wa saa mbili usiku. Alimwona binti mmoja aliyekuwa amevaa rinda na kumpa mgongo. Kwa kuwa mvua ilikuwa inanyesha, Adili aliona bora kumfanyia hisani. Akalisimamisha gari na kumwomba binti yule aingie. Lo! Hakuamini aliyoyaona. Binti alimchomolea bastola. Alipoinua macho kwa siri kumtazama alipigwa na butwaa. Hakuelewa ilikuwaje hata rafiki yake wa kufa kuzikana akaanza kuvaa marinda!

31. Katika aya ya kwanza neno muamala limepigiwa mstari. Maana yake ni:-

A. jengo la kuishi B. upatanisho

C. uelewano D. uhusiano

32. Ni nini ilijenga uhusiano baina ya Adili na mashaka?

A. Rika lao

B. Rika na ujirani wao

C. Ujirani wao

D. Wazazi wao

33. Nyumba ya bamba ni:-

A. Nyumba inayopendeza

B. Nyumba iliyoezekwa kwa mabati

C. Nyumba iliyoezekwa kwa makuti

D. Nyumba iliyoezekwa kwa nyasi

34. Adili na mashaka hawakuifanya elimu mchezo kwa kuwa:-

A. walitaka kuwa watu watajike

B. walikula kiapo kukomboa familia zao

C. walikuwa washindani

D. wazazi hawakuwakidhia maslahi

35. Umaskini ulidhihirika kijiji ufukara kwa:-

A. jina la kijiji

B. kutokuwa na nyumba ya bamba

C. watoto kusoma kwa bidii

D. kupisha mkono kinyani

36. Maisha ya mashaka yaliingia mashakani:-

A. alipojiunga na vijana wasio na maadili

B. alipokuwa rafiki yake Adili

C. Alipokataa kwenda shuleni

D. alipokuwa mwizi na jambazi

37. Kwa nini Adili alijifunga kibwebwe?

A. Ili afanikiwe maishani

B. Ili amsaidie rafiki yake mashaka

C. Ili asitumie mihadarati

D. Ili awe pwaguzi

38. Wazazi wa Adili na Mashaka walifumbwa macho:-

A. na umaskini wao

B. na usomi wa wanao

C. na shughuli alizozifanya mashaka

D. na ahadi ya kupambwa upya maisha yao

39. Lo! Ni mfano wa:-

A. kihusishi B. kihisishi

C. kiigizi D. kiashiria

40. Kutokana na kifungu funzo tunalopata lipo kwenye methali:-

A. Akili nyingi huondoa maarifa

B. Akili ya mtu ndio wendawazimu wake

C. Subira huvuta heri

D. Hata chui ana mkwe

---

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50.</u>***

Ubakaji na dhuluma nyingine zinazokiuka ubinadamu zinafaa kupigwa vita kwa udi na uvumba na kila mtu katika jamii. Ili vita hivi vifanikiwe na sisis kuwa na jamii nadhifu, mkabala wa tatizo hili usiachiwe waathiriwa pekee.

Inasikitisha kwamba kila baada ya sekunde thelathini, mtu mmoja hushikwa kwa nguvu na kudhulumiwa kimapenzi kwa kuhilikiwa utu wake bila hiari yake. Huu ni uozo ulioozeana katika jamii yetu unapaswa kukanwa kwa vinywa vipana; vya watoto na wazee.

Ingawa kumekuwa na tetesi kwamba mitindo ya mavazi ambayo yanaanika maungo ya mabinti ni mojawapo ya kishawishi kwa udhalimu huu hii si kweli asilani. Je, mtoto mdogo, malaika wa Mungu, ambaye hata mwaka hajatimiza duniani humu anajua nini kuhusu mtindo wa mavazi? Isitoshe zama za mababu zetu hakukuwa na mavazi. Watu walitembea uchi wa mnyama isipokuwa kukinga sehemu zao za siri kwa matawi ama ngozi. Lakini waliendeleza na kudimisha maadili. Ukweli ni kwamba binadamu amemwachia shetani kuongoza hulka zake. <u>Ikiwa binadamu hajaunadi urazimu, basi ameuweka rehani.</u>

Utafiti unaonyesha kwamba matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kutazama kanda chafu za video, aidha nyumbani ama kwenye mtandao, kupandisha raghba ya wanaohusika. Hali hii huwaondoa ubinadamu na kuwatia unyama usiowawezesha hata kutofautisha binadamu na wanyama. Wao huchachawa watakachopata mbele yao ikawa ndicho hata kama haramu.

Hata hivyo, zipo njia tete za kuepuka mtego wa wabakaji. Kwanza, si salama mtu kutembea peke yake gizani katika eneo lisilopitwa na watu wengi. Watu wanashauriwa watembee wawili au zaidi, tena wenye kufahamiana. Pili ukuruba baina ya jamaa wa karibu uwe na mipaka. Utafiti unaonyesha kwamba visa vingi vya ubakaji hutekelezwa na jamaa wa karibu. Hivyo basi, mchanganyiko wa malazi ya jinsia zote uwe mwiko kwani mwanzo wa ngoma ni lele.

Ikiwa umepotea njia si salama kumuuliza tu mtu yeyote. Utakayekutana naye. Wengi huenda wale wanaotega windo hivyo ukawa panya kujiingiza mwenyewe mtegoni. Hivyo basi, ni vizuri kupata habari kamili kuhusu mahali unakoenda. Aidha unapokuwa safarini, tahadhari na watu wanaojifanya kuwa karimu na kukushawishi kwa vinywaji au lawalawa ambazo huenda zikawa na dawa za kulevya. Watakuelekeza madanguroni.

Unapokumbana na uovu huo hata hivyo unashauriwa usinawe, usioge au kubadilisha mavazi kabla ya ushahidi kuthibitoshwa na maafisa wa polisi ama madaktari. Aidha ni muhimu uhakikishe kwamba umewaarifu polisi na uchunguzi kufanywa kabla ya mahali pa mkasa kuhitilafishwa. Isitoshe, unafaa kukimbia hospitalini ili upimwe ili kubainisha ukiwa umeambukizwa magonjwa ya zinaa, ukimwi au madhara mengine yoyote uliyosababishwa. Hii itakuwa hakikisho tosha kwamba maambukizo hayo, ukiwemo ukimwi yatazuiliwa yasienee mwilini.

41. Ubakaji ni:-
   A. Tendo la kuchora baka au alama mwilini
   B. Tendo la kumenyana na mtu aliyekuzidi umri
   C. Tendo la kumshika mtu kwa nguvu na kuzini naye bila hiari yake
   D. Uozo ulioozeana katika jamii

42. Kulingana na taarifa, nini haisababishi ubakaji?
   A. Mitindo ya mavazi ya kisasa
   B. Matumizi ya dawa za kulevya
   C. Athari za kanda chafu za video
   D. Ukinga nyeti kwa ngozi

43. Katika zama za mababu zetu:-
   A. ubakaji ulichochewa na ukosefu wa mavazi
   B. dawa za kulevya zilitumiwa hadharani
   C. watu walitembea uchi lakini walidumisha maadili
   D. waliunadi urazini ama kuuweka rehani

44. Kauli <u>ikiwa binadamu hajaunadi urazini basi ameuweka rehani</u> inamaanisha:-
   A. binadamu amekuwa gaidi mkuu
   B. binadamu amekuwa haini
   C. binadamu amekuwa mwadilifu
   D. binadamu amekuwa mchafu kimaadili

45. Kila nusu dakika:-
   A. mtu mmoja hubakwa
   B. watu hutembea katika maeneo hatari
   C. watu husafiri na wabakaji
   D. polisi wanashika doria katika maeneo hatari

46. Zote hizi ni hatua anazofaa kuchukua mwathiriwa wa ubakaji isipokuwa:-
   A. kufua nguo zake kwa kuogopa aibu
   B. kutohitilafiana na mavazi hadi uchunguzi wa polisi ukamilike
   C. kupimwa na kupewa matibabu ya dharura
   D. kupiga ripoti kwa polisi

47. Ni nini ambacho mtu anafaa kufanya awapo safarini?
   A. Kuuliza njia ikiwa amepotea
   B. Kula na kunywa apewacho na abiria mwenzake
   C. Kuwa panya na kujiingiza mtegoni
   D. Kupata habari kamili kuhusu anakoenda

48. Ili kuepuka mtego wa wabakaji:-
   A. usitembee gizani katika eneo lisilopitwa na wengi
   B. Tembea na watu msiofahamiana
   C. Uweke uhusiano wa karibu na jamaa zako
   D. watu wa jinsia tofauti wachanganye malazi

49. Kutokana na kauli ukawa panya kujiingiza mwenyewe mtegoni, tunaweza kuwa na methali:-
   A. paka akitoka panya hutawala
   B. mtego wa panya huingia waliomo na wasiokuwemo
   C. panya wengi hawachimbi shimo
   D. panya hupuliza aumapo

50. Ni kipi kichwa mwafaka kwa taarifa hii?
   A. Sekunde za ubakaji
   B. Ubakaji
   C. Madhara ya ubakaji
   D. Mbinu za ubakaji